JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**Ofisi Ya Waziri Mkuu - TAMISEMI**

**Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa**

Shule ya Sekondari Mzumbe

Phone: 0688687231/0717015950 – MKUU WA SHULE
0769831453/0713482594 – M/MKUU WA SHULE
0753089697/0625496482 – MWALIMU WA MALEZI

P. O. Box 19,
Mzumbe - Morogoro,
Tanzania.
Mzumbesecondarysch@gmail.com

**KUMB.NA.** MVDC/MZUSS/E.2/4/Vol. VI/124

**Ndugu** Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi ..........................................................

**YAH: KUJIUNGA NA SHULE**

Nafurahi kukujulisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga kidato cha **KWANZA** katika shule ya Sekondari Mzumbe mwaka 2026. **Tunampongeza kwa mafanikio hayo.**

Mwanao atatakiwa kujiunga na shule siku ya **Jumamosi tarehe 11/01/2026 tayari kwa kuanza masomo rasmi siku ya Jumanne tarehe 13/01/2026.** Ni vema akafika shuleni kwa wakati ili asipitwe na masomo.

Shule hii ipo katika Wilaya ya Mvomero, Mkoa wa Morogoro. Ipo kilomita 25 kutoka Morogoro Mjini kuelekea Iringa. Kama unatokea njia ya Dar es Salaam au Dodoma teremka Msamvu, panda daladala kuelekea stendi kuu ya mabasi madogo mtaa wa **Mafiga** kwa gharama ya T.Shs 500/= tu, kisha panda daladala inayoelekea Mzumbe kwa nauli ya T.Shs. 1000/= tu. Ukitumia Tax gharama yake ni T.Shs. 5,000/= kutoka Msamvu hadi **Mafiga**, na Tshs. 20,000/= kutoka **Mafiga** kwenda Mzumbe. Ukitokea njia ya Iringa teremkia **Sangasanga** ambapo unaweza kufika Mzumbe kwa daladala nauli yake haizidi sh. 500/= au pikipiki kwa nauli ya shilingi 2,000/=.

Mwanao atapokelewa shuleni endapo atasoma vyema maelelekezo na kukubaliana nayo na kutimiza mambo yaliyomo kwenye viambata vifuatavyo **A – F**

A. Maelezo Maalumu Ya Kujiunga Na Shule
B. Sheria Kanuni Na Taratibu Za Shule.
C. Fomu Ya Utambulisho Wa Mwanafunzi (**fomu hii itajaziwa shuleni baada ya mwanafunzi kufika)**
D. Fomu Ya Kupimwa Toka Kwa Mganga (Medical Examination).
E. Ahadi/Kiapo Cha Mwanafunzi
F. Fomu Ya Malipo Ya Mwanafunzi

Ni matumaini yetu kwamba mwanao atasoma na kuzingatia maelekezo yote na mzazi/mlezi utamtimizia mahitaji yote kabla ya kuripoti shuleni ili kuepuka usumbufu usio wa lazima.

**NB: Mzumbe sekondari ni shule inayopokea wanafunzi wenye ufaulu wa juu hivyo mwanafunzi atapaswa kudhihirisha uwezo huo kwa kufaulu vema katika masomo yake yote.**

..................................................
***Mbaraka M. Kupela***
***MKUU WA SHULE***

HEADMASTER
MZUMBE SECONDARY SCHOOL

## A.MAELEZO MAALUMU YA KUJIUNGA NA SHULE

1 **MAHITAJI MAALUM YA KUZINGATIA**

**I. SARE ZA SHULE**

a. Suruali mbili Dark bluu yenye marinda 2 na upana inchi 16 na iwe na 'turnup'.
b. Suruali mbili damu ya mzee yenye marinda 2 na upana inchi 16 na iwe na 'turnup'.
c. Shati nyeupe mbili mikono mifupi (Tomato).
d. T. Shirt 2 za rangi ya kijivu.
e. Track suit – Bluu bahari isiyo na maandishi.
f. Jezi (bukta na fulana) rangi ya bluu bahari kwa ajili ya michezo.
g. Mkanda mweusi wa ngozi usio na mapambomapambo.
h. Sweta rangi ya Dark blue.
i. Soksi nyeusi.
j. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba vya kufunika visiwe virefu kisigino visivyo vya fasheni
k. Raba za michezo
l. Kandambili kwa ajili ya kuogea tu.
m. Kukodi godoro shilingi 20,000/- kwa mwaka **(magodoro kutoka nyumbani hayaruhusiwi). Fedha ya kukodi godoro iingizwe kwenye akaunti ya shule.**

II. **VIFAA VYA USAFI**:

a. Soft broom 1/ Squeezer 1
b. Brashi ya kusafishia tundu la choo 1
c. Slesha
d. Reki ya plastiki
e. Rimu 2 za karatasi A4 kwa mwaka kila moja. **DOUBLE A/ BRIGHT WHITE MULTIPURPOSE OFFICE PAPER–**pekee.

2. **MAHITAJI YA BWENI**

i. Shuka 3 rangi ya **pink**
ii. Mto na foronya 2 za **pinki**
iii. Chandarua kwa ajili ya kujikinga na mbu ya bluu bahari.
iv. Taulo
v. Nguo za ndani (chupi 12, Bukta ya ndani na vesti nyeupe 5 )
vi. Ndoo moja lita 10
vii. Sanduku imara la bati moja lenye makufuli mawili
viii. Vyombo vya chakula (Sahani, Bakuli, Kikombe, Kijiko, chupa ya chai, anaweza pia kuja na **hot pot** 1 ndogo kwa ajili ya dharura za kiafya ) **visivyo vya plastiki**

3. **MAHITAJI YA TAALUMA**

- Cheti cha kuzaliwa halisi na Nakala

4. **MAHITAJI YA DARASANI**

i. Madaftari 12 (counter Book)
ii. Kalamu/Penseli za kutosha
iii. Mkebe wa hisabati ( Mathematical Set)
iv. Begi imara la kubebea daftari

5. **BIMA YA AFYA**

**Bima ya Afya** ni wajibu/ dhamana ya mzazi hivyo mwanafunzi anatakiwa kuja nayo shuleni kama hana lipia kwenye akaunti ya wazazi **shilingi 50,400/-** ili aje akatiwe shuleni.

Jina la akaunti: **Charity Begins at Home**
Akaunti Namba: **0152339796800**
Jina la Benki: **CRDB**

.

6. Malipo ya kukodi magodoro yalipwe kwenye akaunti ya shule:-

**Jina la Akaunti : Headmaster Mzumbe Secondary School**
**Nambari ya Akaunti : 22101100075**
**Jina la Benki : NMB TAWI LOLOTE**

**NB:**

(i) Mwanafunzi aje na **'PAY – IN – SLIP'** aliyolipia godoro na kumuonesha Mkuu wa Shule siku ya kuripoti.

(ii) Mzazi utakapofika shuleni utakabidhiwa barua ya makubaliano ya wazazi inayoelezea mipango na mikakati ya kuunga mkono juhudi za serikali katika kuinua ufaulu na miundo mbinu ya shule.

## B: SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE

Sheria na kanuni hizi zinazingatia misingi ya HESHIMA, ADABU, UAMINIFU,UTII na TABIA NJEMA kwa ujumla

Wanafunzi wanatazamiwa kuwa mfano mzuri kwa heshima na tabia kauli na vitendo hivyo:

1. Mwanafunzi atasimama anapomsalimu mwalimu, mtumishi wa shule au mtu yeyote aliyemzidi umri
2. Hairuhusiwi kwa mwanafunzi kutumia lugha chafu au ya kihuni popote na wakati wowote hata kwa wanafunzi wenzake.
3. Hairuhusiwi kwa mwanafunzi
   - (a) Kufuga kucha na nywele
   - (b) Kufuga ndevu
   - (c) Kunyoa kipara
   - (d) Kutukana
   - (e) Kutia dawa nywele (curly) na kujichubua ngozi ya mwili kwa madawa
   - (f) Kuvaa vitu kama mapambo mfano Heleni, Mikufu bangili au vitu vya kiimani kama vile Rozali,
   - (g) Kofia, Kanzu, Vilemba, Suruali fupi kwa kuwa Shule hii ni ya **Serikali**.
   - (h) Kuvaa viatu vya soli nene na ndefu
   - (i) Kuvaa kaptura na kandambili kwenye Bwalo la chakula na Ofisi zote za shule
   - (j) Kuvaa suruali chini ya kiuno
   - (k) Kuvaa nguo za mtindo, mfano- model
4. Mwanafunzi atasimama mstari wakati wa kupata huduma
5. Mwanafunzi atanyoosha mkono juu na kusimama anapouliza au kujibu swali
6. Anatakiwa kuwa mtulivu asipige kelele au vitendo vyovyote vitakavyo sababisha usumbufu kwa wengine anapokuwa Darasani Maktaba, bwenini, wakati wa kujisomea (prep) na katika mikusanyiko yoyote mfano paredi nk
7. Mwanafunzi **LAZIMA** awahi na ahudhurie mahali anapotakiwa katika shughuli za shule. Hivyo Mwanafunzi:-
   - A. Aripoti shuleni tarehe ya kufungua shule na kujiandikisha rasmi siku na saa ya kuripoti kwa mwalimu anayehusika.
   - B. Ahudhurie vipindi vyote darasani kama ilivyopangwa
   - C. Ahudhurie kwenye kazi atakazopangiwa
   - D. Ahudhurie kwenye paredi ya uhakiki wa uwepo wake shuleni (Roll call). Ukaguzi wa Usafi , kupandisha Bendera ya Taifa, Mikutano ya nyumba, Mikutano ya darasa na Maabara za shule.
8. **NI LAZIMA** mwanafunzi awe katika sare ya shule na awe na **KITAMBULISHO** kwa nyakati zote awapo shuleni na nje ya shule kama:-
   Anapotoka nje ya shule kwa ruhusa maalumu kwenda Posta, Kanisani, Msikitini, Benki, Hosipitali, likizo au kwa shughuli yoyote itakayomlamzimu kwenda nje ya shule.
9. **NI LAZIMA** mwanafunzi awe ndani ya mipaka ya shule wakati wote isipokuwa akiruhusiwa kuwa nje ya mipaka ya shule kwa ruhusa maalumu, na atapaswa kuwa na kibali (pass) cha maandishi.
10. Mwanafunzi lazima ahudhurie prep inayoanza saa 2.00 jioni na awe kitandani kwake wakati wa kuzima taa (lights out) saa 5:00 usiku.
11. Mwanafunzi haruhusiwi kutumia umeme kwa shughuli yoyote ile awapo bwenini au darasani.
12. Hairuhusiwi kufanya mikutano yoyote shuleni pasipo kibali cha Mkuu wa Shule na ikiwa kibali kimetolewa kikundi au chama kitatakiwa kuandika muhtasari wa kikao na nakala kuwasilishwa kwa Mkuu wa Shule.
13. USAFI: Mwanafunzi anawajibika kuwa msafi kwa mavazi na mwili wake na kushiriki kuyaweka mazingira ya shule katika hali ya usafi.
14. Mwanafunzi anapaswa kuvaa sare za Shule ya Sekondari Mzumbe muda wote akiwa ndani na nje ya shule na achomekee shati lake. **Mavazi yasiyo ya shule hayaruhusiwi kabisa.**
15. Hairuhusiwi kujihusisha na mikutano ya siasa katika kipindi chote awapo mwanafunzi.
16. **MAENEO YASIYORUHUSIWA:**
   Mwanafunzi haruhusiwi kufika/kuingia sehemu zifuatazo bila ruhusa maalumu:
   - a. Ofisi za shule
   - b. Bohari za shule
   - c. Kwenye disco, ngoma , mziki au kwenye sherehe yoyote ndani na nje ya shule
   - d. Maabara
   - e. Baa,kilabuni au mahali popote panapouzwa pombe au vileo vingine
   - f. Nyumba za wageni (Guest House)
   - g. Nyumba za watumishi/walimu

**ZINGATIA:**

Unataarifiwa kuwa shule hii ni shule ya Serikali wala siyo ya **DINI** Fulani. Aidha inazingatia katiba ya nchi kuhusu uhuru wa kuabudu, hivyo wanafunzi huruhusiwa kwenda sehemu za ibada kulingana na imani zao. Pia kumepangwa vipindi viwili vya dini katika ratiba ya masomo kwa siku ya Jumatano na kila siku jioni kabla ya chakula kuanzia saa 12.00 – 01.00 usiku. Wanafunzi hawaruhusiwi kuanzisha ratiba yao ya kuabudu katikati ya vipindi na ratiba zingine za shule. Tofauti ya hayo Mzazi/Mlezi anashauriwa kumtafutia mwanafunzi shule ya seminari endapo mwanafunzi huyo ana wito wa dini husika.

**MAKOSA YANAYOWEZA KUMFUKUZISHA MWANAFUNZI SHULE:**

1. Wizi
2. Uasherati, ushoga na ulawiti,ubakaji
3. Ulevi wa aina yoyote kama utumiaji wa madawa ya kulevya, pombe, sigara,bangi, mirungi n.k
4. Makosa ya jinai
5. Kuoa au kuolewa
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
7. Kupigana au kumpiga mwingine.
8. Kudharau Bendera ya Taifa
9. Kulala nje ya shule bila ruhusa ya Mkuu wa shule
10. Kuchochea au kufanya vurugu, kugoma kwa namna yoyote
11. Kutoa lugha ya matusi
12. Kumdharau kiongozi wa shule, mwalimu, mfanyakazi na jamii kwa ujumla
13. Kutohudhuria vipindi
14. **Mwanafunzi kumiliki simu au sehemu ya simu kama laini, Charger nk**
15. Kupata wastani wa alama 60% katika masomo yake
16. **Kukosa kuhudhuria vipindi darasani na au kutofanya mitihani na majaribio kwa makusudi**

Phone: +255688687231
+255677203197

P. O. Box 19,
Mzumbe - Morogoro,
Tanzania.
Mzumbesecondarysch@gmail.com

# E. MEDICAL CERTIFICATE FORM

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION OF ……………………………………………… FORM ………**

Please examine the above named as to his fitness for admission to school as a student.

***Name and signature of requesting Officer.***

Name ……………………………………………….. Signature ……………………………………………….

Date ……………………………………………

**To be completed by a Government Medical Officer in respect of FORM 1/5 entrants:**
**Pupil's Full Name**……………………………………………………………………………………………………

**Blood count (Red and White)** ……………………………………………………………………………………

**Stool Examination** …………………………………………………………………………………………………

**Urinalysis**……………………………………………………………………………………………………………

**Syphilis Test**………………………………………………………………………………………………………

**T. B. Test**……………………………………………………………………………………………………………

**Eye Test**……………………………………………………………………………………………………………

**Ears**……………………………………………………………………………………………………………………

**Chest**…………………………………………………………………………………………………………………

**Spleen**………………………………………………………………………………………………………………

**Abdomen**……………………………………………………………………………………………………………

**Blood Group**…………………………………………………………………………………………………………

**ADDITIONAL INFORMATION: e.g. Physical defects or impairments infections, chronic or family diseases etc.**

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

I have examined the above named and I consider that he is physically fit/unfit to pursue as stated above.
Name and signature of Certifying Officer.

Name ………………………………………… Signature………………………………………
Station ………………………………………… Designation …………………………………..
Date ………………………………………… STAMP ………………………………………

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
**Ofisi Ya Waziri Mkuu - TAMISEMI**
**Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa**
Shule ya Sekondari Mzumbe

Phone: +255688687231
+255677203197

P. O. Box 19,
Mzumbe - Morogoro,
Tanzania.
Mzumbesecondarysch@gmail.com

### F. AHADI/ KIAPO CHA MWANAFUNZI

Mimi ………………………………………………………………………………………………………………
Ambaye nimechaguliwa kujiunga na **SHULE YA SEKONDARI MZUMBE KIDATO CHA I** mwaka **2026** ninaipokea na kuikubali nafasi niliyo pewa kwa malengo ya kusoma kwa bidii na kufikia malengo ya Taifa na Shule ya Sekondari ya Bweni Mzumbe.

Ninatambua kuwa nafasi hii ni adimu, nyeti na ya upendeleo kwangu ili niweze kusoma na kufanya vizuri katika masomo nikiwa na tabia na mwenendo mwema kwa ajili ya taifa langu la Tanzania, familia yangu na kwa ajili yangu pia.

Nina amini kuwa vitendo vyovyote vinavyopelekea uzembe katika kufanikisha makusudio haya ni hujuma kwa Taifa langu, familia yangu na kwangu pia. Hivyo ninaahidi kuwa, nikiwa hapa shuleni:

i. Nitasoma kwa bidii kwa malengo ya kufanya vizuri katika masomo yangu.
ii. Nitashika na kufuata sheria na taratibu zote za shule kama nilivyo zisoma na kuzielewa na zingine zitakazo kuwa zikitolewa mara kwa mara.
iii. Sitajihusisha na vitendo vyovyote vya utovu wa nidhamu nikiwa hapo shuleni.
iv. **Nitafaulu kaika mitihani yangu yote na kamwe sitapata chini ya alama za ufaulu za shule ambazo ni 60%**
v. Ikiwa nitakiuka sheria kanuni na taratibu za shule kama nilivyo zisoma na kuzielewa, nitakubali kurudi nyumbani kumwita mzazi/ mlezi wangu. ……………………………………………………… ( Jina la mzazi) kwa ajili ya hatua zaidi.

Saini ya mwanafunzi …………………………………… tarehe ………………………………………………………

---

### SEHEMU YA MZAZI/MLEZI

Mimi ……………………………………………………………………… ninakubali mtoto wangu
………………………………………………………………… Kupata na kupokea nafasi katika shule ya sekondari Mzumbe mwaka 2026. Ninaahidi kumpatia mahitaji yote ya shule kama ilivyo katika maagizo ya kujiunga na shule.
Ninakuhakikishia kuwa nitashirikiana na shule wakati wote kuona kuwa mwanangu anatekeleza wajibu wake kwa shule na kwa taifa, ikiwa ni pamoja na kufanya vizuri katika masomo.
Anuani yangu ya kudumu ni ………………………………………………………………..
………………………………………………………………..
Simu ………………………………………………………..
Iwapo nitapata uhamisho wa kubadili makazi nilazima nitaijulisha shule kwa maandishi

Saini ya Mazazi/Mlezi ………………………………………Tarehe ………………………….

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**Ofisi Ya Waziri Mkuu - TAMISEMI**

**Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa**

Shule ya Sekondari Mzumbe

Phone: +255688687231
+255677203197

P. O. Box 19,
Mzumbe - Morogoro,
Tanzania.
Mzumbesecondarysch@gmail.com

## MFANO WA SARE ZA SHULE

### 1. SARE ZA DARASANI





**2. SHAMBA DRESS**



**3. SARE ZA MICHEZO**



